## Tohara kwa Wanaume & kuzuia maambukizi ya VVU

Mwanzo

Mwishoni mwa mwaka wa 2006, ilikadiriwa kuwa watu milioni 39.5 walikuwa wanaishi na virusi vya ukimwi na milioni 4.3 kuambukizwa na virusi kwa mara ya kwanza mwaka huo. Kuzuia ni lazima kupewe kipaumbele katika kukabiliana na UKIMWI na jitihada zinafanyika kutafuta teknolojia mpya za kuzuia ili kuimarisha mbinu ambazo tayari zinajulikana kuwa madhubuti kwa kuzuia. Munamo mwezi Machi mwaka wa 2007, Shirika la Afya Duniani (WHO) na Ushirikiano wa Umoja wa Mataifa juu ya VVU / UKIMWI (UNAIDS) lilipendekeza kwamba mipango na sera za kuzuia VVU zinatambua tohara kwa wanaume kama mkakati wa ziada, muhimu kwa kuzuia wanaume kutoambukizwa VVU kutoka kwa washirika wa kike waliouambukizwa .

Tohara kwa wanaume ni kuondolewa kwa upasuaji kwa yote au sehemu ya govi la uume. Ni mojawapo ya taratibu kongwe na aina ya upasuaji inayo fanywa kwa wingi zaidi duniani kote, ifanyikayo kwa sababu za kidini, kiutamaduni, kijamii au matibabu. Tohara kwa wanaume sasa imepewa tathmini kama njia ya kupunguza maambukizi ya VVU. Hakika, takwimu za aina mbalimbali ya masomo ya uchunguzi ya epidemiological zimeonyesha kwamba tohara inawapa wanaume baadhi ya -si kamili - ulinzi dhidi ya virusi vya ukimwi kwa njia ya ngono kati ya mwanamume na mwanamke.

Hata hivyo, wanaume waliotahiriwa hawawezi kufikiri kwamba hawako hatarini, huu ni ufahamu usio sahihi. Baadhi ya wanaume kwa kutoelewa hufanya uchaguzi ulio hatari zaidi ya kwa sababu ya kutahiriwa kwao, ambao unaashiria ulinzi wowote ambao tohara yaweza kuleta. Ni muhimu kuelewa kwamba tohara siyo ulinzi, lakini njia ya kupunguza uwezekano wa maambukizi.

Matokeo ya Utafiti

Tangu miaka ya 1980, idadi ya tafiti za uchunguzi zinaonyesha kwamba wanaume waliotahiriwa wana kiwango cha chini cha  maambukizi ya VVU kuliko wanaume wasiotahiriwa.

Majaribio ya kwanza ya baghala na yenye kudhibitiwa, yaliofanywa nchini Afrika Kusini, yalionyesha kuwa tohara kwa wanaume hutoa asilimia 61 ya kinga dhidi ya wanaume kupata virusi vya ukimwi kupitia ngono kati ya mwanamume na mwanamke. Majaribio hayo yalisimamishwa mwaka 2005, wakati uchambuzi wa muda ulionyesha kupunguka kwa angalau kiwango cha 60% ya maambukizi ya VVU miongoni mwa watu waliotahiriwa.

Majaribio yaliofanyika Kisumu, Kenya, yalionyesha kuwa tohara hupunguza hatari ya kuambukizwa kwa VVU watu wazima wanaume kwa asilimia 53% . Hayakueleza kama tohara kwa wanaume ina adhari zozote juu ya hatari ya uenzaji wa VVU.
Majaribio yaliofanyika Rakai, Uganda, yalionyesha kuwa tohara hupunguza hatari ya kuambukizwa kwa VVU watu wazima wanaume kwa asilimia 48% . Hayakueleza kama tohara kwa wanaume ina adhari zozote juu ya hatari ya uenzaji wa VVU.

Katika Majaribio yote matatu ya baghala na yenye kudhibitiwa, matukio ya VVU yalikuwa chini mno katika kuingilia (wanaume waliotahiriwa) kuliko katika kundi la kudhibiti (wanaume wasiotahiriwa),

hata hivyo kwa jumla yalibaki kuwa juu (0.7-1.0 kwa kila miaka 100 (ya kutazama kila mshiriki) kwa wanaume waliotahiriwa).

Katika majaribio zaidi, yakiongozwa na watafiti katika Chuo Kikuu cha Johns Hopkins, tathmini ya athari za tohara kwa wanaume kuhusu hatari ya maambukizi ya VVU kwa washirika wa kike kwa sasa inaendelea huko Uganda, na matokeo yanayotarajiwa munamo 2008. athari za tohara kwa wanaume katika kupunguza hatari ya maambukizi ya VVU miongoni mwa wanaume wanaofanya mapenzi na wanaume haijawahi kutaaliwa katika majaribio ya baghala na yenye kudhibitiwa.

Mifumo ya Kibaiolojia

Wataalam wamekuchukuwa mifumo kadhaa iwezekanayo ili kueleza jinsi tohara inaweza kupunguza uwezekano wa wanaume kupata VVU kwa ngono kati ya mwanamume na mwanamke.

- Upande wa ndani ulio na kamasi wa govi la uume una kiwango kikubwa cha seli zinazolengwa na VVU -seli kama vile Langerhans na chembechembe za CD4 + T. Kuondoa govi hupunguza maradufu idadi ya seli zinazolengwa ambazo ni njia ambayo VVU vinaweza kuvamia mwili wa mwanamume.
- VVU na pathogens wengine wanaweza kuishi kwa muda kwenye hifadhi chafu, ndani ya govi ya uume. Kuondoa mazingira haya hupunguza uwezo wa pathogens kuishi.
- Mikwaruzo na uvimbe wa tishu lainifu ya govi wakati wa kujamiiana ihuwa inawezesha uvamizi wa VVU mwilini. Tohara huondoa govi na kufunga njia hii ya virusi.
- Aidha, tafiti zinaunganishwa tohara kwa wanaume na kiwango cha maambukizi ya chini ya kaswende na baadhi ya magonjwa ya zinaa (STIs) yanayo sababisha vidonda kwenye sehemu za siri na pia kuongeza hatari ya maambukizi ya VVU. Kwa mfano, utafiti nchini Tanzania uligundua kwamba kiwango cha wanaume waliotahiriwa kimepungua kwa nusu katika maambukizi ya kaswende ikilinganishwa na wenzao wasiotahiriwa.

Matokeo ya sera

Inatarajiwa kwamba habari ya matokeo haya hata ongeza mvuto katika tohara kwa wanaume kutoka kwa serikali, taasisi zisizo za kiserikali, na wananchi kwa ujumla katika nchi kadhaa, pamoja na kuongeza mahitaji ya huduma za wanaume kutahiriwa. Serikali zinazozingatia jinsi ya kuboresha upatikanaji wa huduma salama za tohara kwa wanaume zahitaji kufikiria jinsi ya kuweka shambamba tohara kwa wanaume ndani ya programu pana ya kuzuia maambukizi ya VVU. Wakati huo huo, hatari ya tohara zisizo salama ni ya juu kama usalama hautapewa kipaumbele. Baada ya kuzingatia maadili, haki za binadamu, fedha, wafanyakazi waliofuzu, usalama na masuala mengine, nchi zilizouamua kupanua huduma za tohara kwa wanaume zitahitaji kuhakikisha kwamba inaendelezwa kwa njia iliyokubalika kitamaduni na kwamba inatekelezwa kwa njia salama.

Hitimisho

Ushahidi wa utafiti kwamba tohara kwa wanaume inapunguza maambukizi ya VVU kupitia ngono kutoka kwa wanawake na wanaume ina msukumo. Sehemu ya kinga inayotolewa na tohara kwa wanaume imeonekana thabiti katika masomo ya uchunguzi (ya kiikolojia, kisehemu na yenye

kushirikisha) na tatu ya majaribio ya baghala na yenye kudhibitiwa yaliofanywa katika mazingira mbalimbali.

Hata hivyo, tohara kwa wanaume si kinga kamili kutoa dhidi ya maambukizi ya VVU. wanaume waliotahiriwa bado wanaweza kuambukizwa na virusi vya ukimwi, na kama tayari wana VVU, wanaweza kuambukiza wapenzi wao. Kukuza na kutoa usalama wa tohara kwa wanaume haichukui nafasi ya hatua zingine za kuzuia maambukizi ya VVU kwa ngono kati ya jinsia mbalimbali lakini inatoa mkakati wa ziada. tohara kwa wanaume kamwe haiwezi kuchukua nafasi ya mbinu zingine zinazojulikana za kuzuia VVU na lazima iwe inachukuliwa kama sehemu ya mkakati kamilifu wa kuzuia VVU.

Aidha, ni muhimu ili kuhakikisha kwamba taarifa za wazi na sahihi pamoja na mikakati ya mawasiliano ya ngazi ya kimataifa, kikanda na kitaifa, juu ya haja ya kuendelea na hatua zingine za kuzuia VVU. Hii itakuwa muhimu ili kuzuia wanaume kuendeleza hisia za uongo za kuwa salama na kujihusisha na tabia hatari ya ngono ambayo inaweza kudhoofisha sehemu ya kinga inayotolewa na tohara kwa wanaume.

Wakati huo huo, kukuza tohara kwa wanaume kama njia ya kuzuia VVU inahitaji:

* tohara kwa wanaume lazima ifanywe sehemu ya mpango mpana wa kuzuia VVU
* Ipo haja ya kuimarisha Huduma za afya ili kutoa huduma bora iliyo salama
* Wenye kupanga mipango lazima wahakikishe kwamba tohara kwa wanaume inatambua haki za binadamu za mteja
* huduma iliyokubalika Kitamaduni

**Resources:**


WHO. *WHO and UNAIDS announce recommendations from expert consultation on male circumcision for HIV prevention* http://www.who.int/hiv/mediacentre/news68/en/index.html

WHO, UNAIDS. *New Data on Male Circumcision and HIV Prevention: Policy and Programme Implications: Conclusions and Recommendations* http://www.who.int/hiv/mediacentre/MCrecommendations_en.pdf.

WHO. *Information Package on Male Circumcision and HIV Prevention;* http://www.who.int/hiv/mediacentre/infopack_en_1.pdf

UNAIDS, WHO. *Male Circumcision and HIV: Recent Developments;* http://data.unaids.org/pub/FactSheet/2007/20061229_mc_fs_en.pdf?preview=true

Advocates for Youth. Written by Kathy Osborn http://www.advocatesforyouth.org/publications/factsheet/fsmalecircumcision.htm